Toleo Na.: 003

# JARIDA LA USHIRIKA

Jarida la Tume ya Maendele ya Ushirika Tanzania
ISSN 2714 - 2175
JULAI - SEPTEMBA 2020



*"Ushirika - Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| 3 | Kutoka kwa Mrajis na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika |
| 4 | Makamu wa Rais ahimiza Matumizi ya Stakabadhi za Ghala |
| 6 | Mfumo wa TEHAMA Kuimarisha SACCOS Nchini |
| 8 | Habari Picha Katika "Kijiji Cha Ushirika" - Maonesho ya Nanenane, Simiyu |
| 9 | Ushirika waleta Neema ya Pembejeo kwa Wakulima |
| 12 | CHAURU Inavyonogesha Ushirika Mkoani Pwani |
| 13 | TCDC yapokea Pikipiki kutoka CRDB BANK |
| 15 | Maswali na Majibu Kuhusu Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Katika Usimamizi wa Saccos Nchini |
| 16 | Mikakati ya Tume Katika Kuendeleza Viwanda |
| 18 | Mifumo ya Kuwezesha Upatikanji wa Fedha Kwa Vyama vya Ushirika wa Nyumba |
| 20 | Mwongozo wa Makisio ya Mapato na Matumizi kusaidia Usimamizi Katika Vyama vya Ushirika |

# KUTOKA KWA MRAJIS NA MTENDAJI MKUU WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA



**Dkt. Benson Ndiege**
Mrajis wa Vyama vya Ushirika na Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania

Katika kusimamia biashara ya Huduma Ndogo za Fedha na kuhamasisha ukuaji na uendelezaji wa Sekta hiii, Serikali ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018. Aidha, Serikali ilitunga Kanuni za Jumla na Kanuni mahsusi za biashara ya Huduma Ndogo za Fedha za Mwaka 2019 kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa Sheria husika.

Benki Kuu ya Tanzania (BOT) imepewa jukumu la kusimamia taasisi zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha nchini kwa kushirikiana na mamlaka nyingine kama Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Serikali za Mitaa. BOT ilikasimisha mamlaka na majukumu yake katika kusimamia SACCOS kwa (TCDC) Novemba 22, 2019 kwenye Gazeti la Serikli - GN.887. Mwezi Desemba 2019, BOT ilitoa tangazo kwa umma kuelekeza SACCOS zote kutakiwa kuanza kuomba leseni kupitia kwa Maafisa Ushirika (W) pamoja na Warajis Wasaidizi (M).

## MAELEKEZO KWENYE SACCOS

Katika kutekeleza Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018, kila SACCOS zinapaswa kuhakikisha zinafanya mapitio ya nyaraka zilizoandaliwa na kufanya maboresho kwenye nyaraka hizo kwa lengo la kukamilisha nyaraka husika na kuidhinishwa.

Kushindwa kukamilisha nyaraka hizi na kuidhinishwa na Mrajis, SACCOS zitashindwa kuomba na kupata leseni kwa mujibu wa Sheria. Hivyo, ni vyema kukamilisha nyaraka hizi mapema na kuanza mchakato wa kuomba leseni ili kuepuka adhabu zinazoweza kutozwa kwenye SACCOS.

Ni lazima kila SACCOS ifuate Utaratibu wa kuomba Leseni ambapo Leseni zote zinatolewa na Mrajis wa Vyama vya Ushirika nchini Makao Makuu ya Tume. Warajis Wasaidizi wa Mikoa na Maafisa Ushirika wa Wilaya wanasaidia kutoa maelekezo na kufanya tathmini ya maombi ya leseni zilizoombwa na SACCOS.

Maombi yote ya leseni yataombwa kwa njia ya mtandao (SACCOS License Online Application System).

SACCOS zimegawanywa katika makundi mawili ya leseni -SACCOS zenye leseni daraja A na daraja B. Kiwango cha chini cha mtaji kwa SACCOS zenye leseni daraja A ni Tsh Milioni 10 na leseni daraja B ni Tsh Milioni 200.

SACCOS haitaruhusiwa kutoa huduma ndogo za fedha pasipo kuwa na Leseni ya utoaji wa huduma hizo kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Huduma ndogo za fedha. Iwapo SACCOS itashindwa kufikia kiwango cha chini cha mtaji, SACCOS hiyo itapaswa kuwasilisha mpango wa kuongeza mtaji ndani ya siku 60 tangu ishindwe kufikia mtaji huo kwa Msimamizi.

# MAKAMU WA RAIS AHIMIZA MATUMIZI YA STAKABADHI ZA GHALA



*Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan, Akisoma hotuba yake wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane Nyakabindi Mkoani Simiyu*

Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ametoa wito kwa wakulima wa mazao mbalimbali nchini kuongeza matumizi ya Mfumo wa Ushirika kwa kutumia Stakabadhi za Ghala ili kupata uhakika wa masoko na bei zenye tija kwa wakulima.

Makamu wa Rais ameyasema hayo wakati wa akizindua Maadhimisho ya Maonesho ya Kilimo na Sherehe za Wakulima NaneNane, Kitaifa leo Agosti 01, 2020 katika Viwanja vya Nyakabindi, Mkoani Simiyu.

Makamu wa Rais amesema kuwa ni muhimu wakulima kuuza mazao yao kupitia vyama vya Ushirika nchini hususan maeneo ambayo tayari yana mifumo imara ya Stakabadhi za Ghala. Aidha, ametoa wito kwa mikoa yote kujiandaa vyema na matumizi ya mifumo ya Ushirika na Stakabadhi za Ghala ili kupata bei zenye tija na zenye manufaa kwa wakulima.

Akizungumzia kuhusu kauli mbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu 2020, isemayo "Kwa maendeleo ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Chagua viongozi Bora 2020", Mama Samia amesema kuwa inaendana na kipindi hiki ambacho tunaelekea Uchaguzi Mkuu wa Viongozi mbalimbali nchini. Hivyo wananchi watumie fursa hiyo kuchagua viongozi bora watakaoleta mapinduzi chanya katika Sekta za Uchumi wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

"Wakati wa uchaguzi utakapofika tumieni fursa hiyo kuchagua viongozi watakaoleta mapinduzi chanya kwa kusimamia Sera, uhakika wa masoko na maslahi mapana ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na maendeleo ya Taifa," alisema Mhe. Samia.

"Tumeimarisha masoko ya mazao ya kilimo kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghalani. Serikali imeimarisha mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwa kuhakikisha mazao yanauzwa kwa mfumo huo kupitia vyama vya ushirika ili kuwapatia wakulima masoko ya uhakika na bei zenye tija," alisisitiza Makamu wa Rais Katika uzinduzi huo Waziri wa Kilimo, Mhe. Japhet Hasunga,

alitaja baadhi ya maeneo ambayo Serikali imeendelea kuweka msukumo wa maendeleo ya kimkakati ni pamoja na usajili wa wakulima kwaajili ya upatikanaji wa takwimu sahihi, kujua maeneo ya wakulima, mahitaji yao kwaajili ya kuongeza ufanisi wa uzalishaji wa mazao. Sambamba na hilo Mhe. Hasunga amesema kuwa Serikali inafanya mapitio ya Sera ya Kilimo ya mwaka 2003 kwa lengo la kuanzisha Sheria ya Kilimo, uzinduzi wa Bima ya mazao, uimarishaji wa masoko ya mazao ya kilimo, uimarishaji wa mifumo ya upatikanaji wa pembejeo za kilimo sahihi kwa wakati.



*Baadhi ya wananchi na viongozi mbalimbali wakisikiliza hotuba ya Makamu wa Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Nanenane Mkoani Simiyu wakati wa Ufunguzi wa Maadhimisho ya Sikukuu ya Wakulima Nanenane*

# MFUMO WA TEHAMA KUIMARISHA SACCOS NCHINI




*Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu- Uwekezaji Mhe. Anjelah Kairuki akieleza jambo wakati wa Siku Maalum ya Ushirika wakati wa Maadhimisho ya Nanenane Mkoani Simiyu*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) iliyoundwa kwa Sheria ya Vyama vya ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 kwa lengo la kusimamia na kuhamasisha maendeleo ya sekta ya ushirika nchini, husimamia aina zote za Vyama vya Ushirika ikiwemo vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya ushirika pamoja na Kanuni zake. SACCOS zimeanza kusimamiwa pia kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2018 pamoja na Kanuni zake za mwaka 2019 kutokana na kutungwa kwa Sheria na Kanuni zake kwa lengo la kuimarisha, kusimamia na kuendeleza sekta ya biashara ya Huduma Ndogo za Fedha zinazotolewa na watoa huduma ndogo za fedha nchini zikiwemo SACCOS. Serikali kupitia TCDC na Benki Kuu imedhamiria kusimamia kwa ufanisi vyama vya ushirika wa Akiba na Mikopo kwa kuweka mifumo madhubuti, itakayowezesha upatikanaji wa Taarifa sahihi kutoka kwenye vyama hivyo. Taarifa hizo zitasaidia kutambua maendeleo na changamoto za vyama, na kutoa ushauri wa namna ya kuboresha mipango yao.

SACCOS nyingi nchini zimekuwa zikikabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo mitaji midogo, idadi ndogo ya wanachama, uwekezaji mdogo wa hisa, Akiba na Amana, kucheleweshwa kurejeshwa kwa mikopo kwa wakati, uandishi na utunzaji usioridhisha wa hesabu na kumbukumbu za Vyama, weledi mdogo kwa baadhi ya viongozi na watendaji wa Vyama, ubunifu, uaminifu, ukiukwaji wa Sheria, Kanuni, Sera, miongozo ya Vyama. Vilevile SACCOS zimekuwa na changamoto katika kuweka matengo kwenye akaunti maalum, kutoainishwa kwa umri wa mikopo pamoja na kutotumia mifumo mizuri ya kutunza kumbukumbu ya TEHAMA.

Kwa kuzingatia changamoto hizo pamoja na maboresho mbalimbali yanayofanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) katika usimamizi na utoaji wa huduma kwenye SACCOS, imeweza kutengeneza mfumo wa uombaji na utoaji wa leseni kwa njia ya mtandao kwa lengo la kupunguza changamoto za uwepo wa SACCOS zisizokuwa na tija ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa SACCOS hizo.

Hivi Karibuni wakati wa Maonesho ya Wakulima Nanenane Kitaifa tarehe 03 Agosti, 2020 Siku ya kuhamasisha Ushirika nchini, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiwakilishwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu – Uwekezaji Mhe. Anjellah Kairuki alizindua Mfumo huo wa TEHAMA kwa ajili ya uombaji na utoaji wa leseni kwenye Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS). Mfumo huo unaojulikana kwa jina la SACCOS Lisence Online Application System, unapatikana kwenye tovuti ya Tume ya Maendeleo ya Ushirika (www.ushirika.go.tz) sehemu iliyoandikwa License Application.

Mrajis wa Vyama vya Ushirika ambaye pia ni Mtendaji Mkuu wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Dkt. Benson Ndiege, amesema Mfumo wa SACCOS Lisence Online Application System unalenga kuboresha usimamizi na udhibiti wa shughuli za SACCOS, kuongeza wigo wa SACCOS kuendesha shughuli zake kwa kutoa huduma mbalimbali za kifedha, SACCOS kujiendesha kwa weledi na kusimamiwa na viongozi na watendaji wenye sifa ambao watasaidia kubuni bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya kukidhi matakwa ya wanachama wake na kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati.

Dkt. Ndiege amezikumbusha SACCOS kufuata Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha ambazo zimeshaanza kufanya kazi tangu tarehe 01 Novemba, 2019. “Muda wa mpito uliotolewa kwenye Sheria ni mwaka mmoja yaani kuanzia tarehe 01 Novemba 2019 hadi 31 Oktoba 2020. Hivyo, SACCOS zote zinapaswa kuhakikisha zinaomba na kupewa leseni ndani ya muda ulioelekezwa Kisheria,” alisisitiza Dkt. Ndiege



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Uwekezaji Mhe. Anjellah Kairuki akizindua Mfumo wa TEHAMA wa uombaji wa Leseni kwa Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) kwa niaba ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia Mhe. Kassim Majaliwa, kushoto ni Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege, Waziri wa Kilimo Mhe. Japhet Hasunga na Katibu Mkuu Kilimo Gerald Kusaya (katikati) wakishuhudia tukio hilo wakati wa Maadhimisho ya Nanenane Kitaifa Mkoani Simiyu.*

# HABARI PICHA KATIKA "KIJIJI CHA USHIRIKA" MAONESHO YA NANENANE, SIMIYU




*Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU) akimuelezea shughuli zinazofanywa na CHAURU mwananchi aliyefika katika maonesho ya Wakulima Kitaifa yaliyofanyika katika Viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu*




*Mfanyakazi wa Shirika la Agricom Remmy Nditti (kulia) akielezea shughuli za Shirika hilo pamoja na matumizi ya zana za Kilimo kwa Mrajis wa Vyama vya Ushirika Dkt. Benson Ndiege*




*Wananchi mbalimbali waliofika kupata elimu ya Fedha katika banda la Maonesho la Shirika lisilo la Kiserikali la SBFIC katika Kijiji cha Ushirika*



*Mfanyakazi wa Chama Kikuu cha Ushirika KNCU akitoa huduma ya Kahawa kwa wananchi mbalimbali waliofika katika Banda hilo kujifunza shughuli za Ushirika wa Kahawa kutoka Kagera*

## USHIRIKA WALETA NEEMA YA PEMBEJEO KWA WAKULIMA




*Sehemu ya Mifuko ya Mbolea iliyoagizwa kwa Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea kwa Pamoja (BPS) iliyoagizwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Iringa Farmers Mkoani Iringa*

Ushirika umetajwa kuwa ni moja ya chachu ya kuleta mabadiliko chanya miongoni mwa wakulima kutokana na kuanza kutumia mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (PBS) hivi karibuni. Hayo yamesemwa na Victor Mwipopo Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima wa Iringa (Iringa Farmers' Cooperative Union) leo Ijumaa Agosti 21, 2020 wakati akieleza namna Chama hicho kilivyofanikiwa kufanya uagizaji na usambazaji wa mbolea kwa wakulima wao mkoani Iringa.

Mwenyekiti huyo alieleza kuwa kwa mara ya kwanza Chama hicho katika msimu wa kilimo 2020/21 Chama Kikuu hicho kimeanza kutumia mfumo wa ununuzi wa Mbolea kwa pamoja. Alifafanua kuwa Chama hicho kiliagiza mbolea ya kupandia (DAP) na mbolea ya kukuzia (UREA) kiasi cha Tani 274 ambazo tayari zimeshasambazwa kwa wakulima katika vituo maalum vyenye maghala vikiwemo Lupembelwasenga, Kilolo, Ikimilinzowo na Isalavanu mkoani Iringa.

"Utaratibu unaotumika kusambaza mbolea hizo ni kuuza kwa pesa taslimu kwa mkulima yeyote mwenye uwezo wa kununua lakini kipaumbele cha kwanza ni mkulima mwanachama wa Ushirika ili kumuwezesha kupata pembejeo hizo kwa gharama nafuu," alisema Mwenyekiti Meneja wa Chama Tumaini Lupola akifafanua zaidi kuhusu mfumo huo alieleza kuwa bei za mbolea hizo zimepangiwa bei elekezi ambayo ni Sh. 50,000 kwa DAP na Sh. 43,500 kwa UREA kwa mfuko wa Kilo 50 kwa wanachama wa Ushirika. Meneja akieleza kuwa awali wakulima wamekuwa wakinunua kwa Mawakala na wafanyabiashara kwa bei kubwa zaidi pamoja na mikopo ya riba kubwa, jambo ambalo limekuwa likiongeza gharama za uzalishaji kwa wakulima.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea (TFRA) ameeleza kuwa Mfumo huo ulianzishwa kwa Kanuni ya mwaka 2017 kwa lengo la kuimarisha ubora wa mbolea na kuhakikisha wakulima wanapata pembejeo hiyo kwa bei nafuu na kwa wakati.

Nae mkulima mkoani Iringa Betty Mwikanalo mkulima wa Chama cha msingi cha Ushirika cha Lupembelwasenga AMCOS ameshukuru sana kwa Chama hicho cha Msingi kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika cha Iringa Farmers' Cooperative Union kwa uagizaji huo wa pamoja kwani mbolea imewafikia kwa wakati tofauti na misimu mingine mbolea hufika kwa kuchelewa na mara nyingine kuingiliana na shughuli nyingine za kilimo. Amepongeza hatua hiyo ambalo itafanikisha kufanya kilimo chenye tija zaidi.



*Mwenyekiti wa Chama Kikuu cha Ushirika Iringa Farmers Bw. Victor Mwipopo (katikati) akisikiliza majadiliano ya wajumbe wa Bodi ya Chama hicho kuhusu masuala ya uagizaji wa Mbolea kwa Pamoja (BPS)*

## MAJUKUMU YA MWANACHAMA KATIKA CHAMA CHA USHIRIKA

(i) Kusimamia uendeshaji wa shughuli za chama cha ushirika;

(ii) Kuhakikisha hesabu za chama cha ushirika zinaandaliwa kwa wakati;


(iii) Kutoa mawazo mbalimbali katika kuboresha utendaji wa chama;

(iv) Kushiriki vikao na mikutano mbalimbali kwa mujibu wa kanuni na taratibu za ushirika; na

(v) Kulipa malipo ya hisa zinazohitajika, kiingilio na michango mingine inayohitajika.

Kwa mawasiliano zaidi:
Mrajis wa Vyama vya Ushirika,
Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania,
S.L.P 201
Dodoma
Simu: +255 262322456/ 2322993
tovuti: ushirika@ushirika.go.tz

# Ushirika Sekta Mtambuka



# CHAURU INAVYONOGESHA USHIRIKA MKOANI PWANI

Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji (CHAURU) ni kati ya Vyama vya Ushirika vinavyofanya kazi kwa malengo ya kuboresha hali ya maisha ya wanachama wake kupitia Kilimo cha Kisasa cha mazao ya biashara na chakula kwa njia ya umwagiliaji pamoja na mvua kulingana na hali ya hewa kilichopo Ruvu Nafco, Kata ya Vigwaza Halmashauri ya Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani.

Hayo yanabainishwa wakati wa mahojiano maalum na Mwenyekiti wa CHAURU Sadala Chacha ambaye akielezea kwa ufupi Chama hicho alisema Chama hicho kiliandikishwa tarehe 19/10/2002 kwa Nambari CR.360 kwa madhumuni makuu ya kuboresha hali ya maisha ya wanachama na familia zao. Chacha alieleza kuwa miongoni mwa majukumu ya Chama hicho ni pamoja na kumiliki maeneo ya mashamba kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, kutafuta na kumiliki majengo na maeneo ya mashamba na makazi kwa niaba ya wanachama, kujihusisha na shughuli nyingine za kiuchumi kwa manufaa ya wanachama wake pamoja na kuhamasisha wananchi na wakazi wa maeneo jirani na chama kujiunga na Chama.

Mwenyekiti alifafanua kuwa kwa sasa CHAURU inajishughulisha zaidi na kilimo na uzalishaji wa mpunga pamoja na Korosho. Huku akitoa wito kwa vijana kutumia fursa ya kilimo hicho kujiajiri na kujipatia kipato.

"Kuna mnyororo wa kazi nyingi zinazoambatana na shughuli za Kilimo. Hivyo, kijana anaweza kuchagua ni sehemu ipi ya kilimo atakayotaka kufanya mfano uzalishaji wa mazao shambani, uvunaji, ufungashaji mpaka uuzaji, vijana waamke karibuni mzione na kuzitumia fursa tulizonazo hapa kwetu Ruvu," alisema Chacha

Awali Mhandisi katika miradi ya Umwagiliaji CHAURU Robert Baltazar alieleza kuwa CHAURU imepiga hatua ya kumiliki Mashine ya kukoboa mpunga ambayo ina uwezo wa kukoboa Tani 3 kwa saa na kutoa mchele ulio katika madaraja tofauti. Hatua ambayo inaongeza thamani ya mpunga. Hivyo, kuongezeka kwa mapato kwa Chama kwa kuuza mchele uliotayari kutumika pamoja na pumba za mifugo kwa wadau mbalimbali.



*Mhandisi Robert Baltazar akionesha jinsi mashine za kukoboa Mpunga za Chama cha CHAURU zinavyofanya kazi katika kiwanda cha kukoboa mpunga kilichopo Ruvu*



*Baadhi ya magunia ya mpunga pamoja na mchele kutoka CHAURU katika Kiwanda cha Kukoboa mpunga Ruvu yakiwa tayari kwa ajili ya kuuzwa kwa wateja*

# TCDC YAPOKEA PIKIPIKI KUTOKA CRDB BANK

Kushirikiana miongoni mwa wadau wa Ushirika ni moja ya misingi ya Ushirika. Tume ya Maendeleo ya Ushirika imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha kuwa inendeleza na kuishi katika msingi wa ushirikiano baina ya Wadau mbalimbali wa Maendeleo ya Ushirika.

Katika jitihada za kuhakikisha kuwa Wanaushi miezi ya karibuni Benki ya CRDB kama sehemu ya wadau wa Ushirika na Maendeleo wameunga mkono juhudi za Ushirika kwa kutoa Pikipiki sita mkoani Katavi kwaajili ya usafiri kwa maafisa Ushirika ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Ushirika.



*Mrajis Msaidizi wa Mkoa wa Katavi, Kakozi Ibrahim ( Kushoto) akipokea funguo za Pikipiki kutoka kwa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi, TCDC - Amina Lyamaiga*

# SACCOS NYENZO YA KUONDOA UMASKINI NCHINI



*Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda akiongea wakati wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanachama wa Ushirika wa Akiba na Mikopo wa K.K.T Arusha Road Ltd, Jijini Dodoma*

Waziri Mkuu Mstaafu Mhe. Mizengo Pinda amesema Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ni chachu ya kuondoa umaskini nchini kutokana na uwezo wa vyama hivyo kuwafikia wananchi wengi na kutoa fursa ya kujiendeleza kiuchumi.

Mhe. Mizengo Pinda ameyasema hayo wakati wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo cha K.K.K.T Arusha Road Limited kilichopo Jijini Dodoma, Septemba 26, 2020.

Akiongea katika Mkutano Mkuu huo Mhe. Pinda amepongeza jitihada zilizofanywa na Chama hicho katika kuwaaunganisha watu wa makundi mbalimbali pamoja kuanzisha Ushirika huo ambao unawezesha watu kutumia uwezo wao wenyewe kuendesha na kuinua uchumi wao wenyewe. “Kwa kutumia Chombo hiki mnaweza kufanya mambo makubwa kiuchumi na mifumo kama hii inaungwa mkono na Serikali kwani ni sehemu muhimu inayochangia kuleta mageuzi chanya ya Kiuchumi, hivyo kuondokana na umaskini,” alisema Mhe. Pinda Waziri Mkuu Mstaafu huyo alisisitiza Vyama vya Ushirika kuendelea kuzingatia misingi ya Ushirika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na taratibu ili kuongeza uendeshaji wa Ushirika wenye Uwazi na kuendelea kutunza imani ya Wanachama katika vyama vyao. Aidha, alisistiza suala la Uwajibikaji wa kila mwanachama katika chama kwani wanachama ndio nguzo na wamiliki wakuu wa Chama. Akitolea mfano suala la Wanachama kuhudhuria vikao kwa mujibu wa masharti na Kanuni za Ushirika. Akisoma taarifa ya Chama Mwenyekiti wa Chama hicho Ibrahim Sumbe amesema Chama hicho kilichoanzishwa mwaka 2004 kilianza na wanachama 89 ambao wameongezeka hadi kufikia wanachama 653.

Mtaji wa Chama umeendelea kukua toka Shillingi 1,701,320 na kufikia kiasi cha Shillingi 646,585,087 mwezi Agosti 2020. Hisa zenye thamani ya Shillingi 514,420,000 Akiba za kiasi cha Shillingi 997,881,503 na Amana za Shillingi 190,002,424.

Akiongeza kuwa Chama hicho kimekuwa kikihudumia wanachama wake kwa kutoa mikopo ya aina mbalimbali ikiwemo mikopo ya biashara, mikopo ya ufugaji, elimu, dharura jamii, dharura ya biashara, ujenzi pamoja na Mikopo ya viwanja. Akifafanua kuwa Chama hicho tayari kimetoa mikopo yenye thamani ya Shillingi 14,226,370,500 kwa wanachama wake.

Kwa upande wake mwanachama Emmanuel Ulomi amesema Mikutano hiyo ni fursa kwa wanachama kujua masuala mbalimbali ya uendeshaji wa Chama chao ikiwemo kusomwa na kupitishwa kwa muhtasari wa Mkutano uliopita, taarifa ya Bodi ya Uongozi, kujadili taarifa ya Kamati ya Usimamizi, kujadili taarifa ya Mkaguzi wa Hesabu za Chama, kujadili na kupitisha makisio ya mapato na matumizi ya 2021 na mambo mengine mengi yenye maslahi kwa wanachama.



*Baadhi ya Wanachama wa Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo wa K.K.T Arusha Road wakifuatilia hotuba na taarifa mbalimbali wakati wa Mkutano Mkuu wa 16 wa Wanachama wa Chama hicho, Jijini Dodoma*

# MASWALI NA MAJIBU KUHUSU SHERIA YA HUDUMA NDOGO ZA FEDHA KATIKA USIMAMIZI WA SACCOS NCHINI

(I) Je, Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha imetungwa lini na kwa lengo gani?
Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilitunga Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha Na.10 ya mwaka 2018 ili kusimamia biashara ya Huduma Ndogo za Fedha na Kuhamasisha ukuaji na uendelezaji wa Sekta hiyo.

(II) Je, ni lini Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ilianza kufanya kazi rasmi?
Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha zilitangazwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuanza kazi rasmi tarehe 01 Novemba, 2019

(III) Je, mtaji wa SACCOS zenye Leseni daraja A na B unaanzia kiasi gani?
Kiwango cha chini cha mtaji wa SACCOS daraja A ni Shillingi Millioni 10 na Shillingi Millioni 200 kwa daraja B

(IV) Je, SACCOS zote zinapaswa kuwa na Leseni kwa mujibu wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha?
SACCOS kama taasisi nyingine za fedha zinatoa Huduma Ndogo za Fedha zinapaswa kusimamiwa na kuzingatia matakwa ya Sheria

(V) Je, ni shughuli gani zinazoruhusiwa kufanywa na SACCOS daraja A kwa mujibu wa Sheria?
Kupokea hisa za Wanachama na za hiari, kupokea Akiba na Mikopo kwa wanachama wake, kufanya uwekezaji, kufanya shughuli nyingine zilizokasimishwa na Benki Kuu na Tume ya Maendeleo ya Ushirika

(VI) Je, ni shughuli gani zinazoruhusiwa kutolewa na SACCOS daraja B kwa mujibu wa Sheria?
Shughuli zote zilizoruhusiwa na SACCOS daraja A, kupokea Amana

(VII) Je, Kwani Saccos Zote Zinapaswa Kupe-wa Leseni Kwa Mujibu Wa Sheria Ya Huduma Ndogo Za Fedha?
SACCOS kama taasisi nyingine za fedha zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha zinapaswa kusimamiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sheria hiyo kwa lengo la kupunguza changamoto za utoaji wa huduma za fedha pamoja na kuimarisha utendaji kazi wa SACCOS nchini.

(VII) Je, Ni Shughuli Gani Zinazoruhusiwa Kutolewa Na Saccos Yenye Leseni Daraja A Kwa Mujibu Wa Sheria?
- Kupokea hisa za uanachama na za hiari
- Kupokea akiba na kutoa mikopo kwa wanachama wake.
- Kufanya uwekezaji
- Kufanya shughuli nyingine zitakazoidhin-ishwa na Benki Kuu au Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

XIII) Je, Ni Nyaraka Gani Zinatakiwa wa kati Wa Kuomba Leseni Daraja B?
SACCOS inapaswa kuwasilisha nyaraka zifuatazo;
- Nyaraka zote zinazotakiwa kwa ajili ya kuomba leseni daraja A.
- Mpango wa Biashara wa miaka (3)
- Sera za Rasilimali Watu, Akiba, Ukwasi, Fedha na Ukusanyaji Madeni.
- Miongozo ya Udhibiti wa Ndani
- Ushahidi wa uwepo wa bima
- Uthibitisho wa malipo ya ada ya sh.300,000 kwa ajili ya maombi ya leseni daraja A

IX) Je, Leseni Itakuwa Inaombwa Na Ku-tolewa Kila Mwaka? Na Je, Itakuwa Ikili-piwa Ada Ya Leseni Kwa Kila Mwaka Pia?
Leseni itatolewa mara moja tu na itadumu muda wote ambao SACCOS itakuwa inatoa huduma zake kwa wanachama kwa kuzingatia matakwa ya She-ria. Leseni hiyo haitalipiwa ada yoyote ya mwaka husika.

## MIKATATI YA TUME KATIKA KUENDELEZA VIWANDA

TCDC inaendelea kutekeleza mpango wa kuhamasisha uanzishaji na ufufuaji wa viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika kwa ajili ya uongezaji thamani . Katika mwaka 2019/2020 tathimini ya viwanda vya kuchakata Pamba ulifanyika na kuonekana kuwa viwanda vingi havina hali nzuri ya kuweza kuchakata Pamba kutokana na uchakavu wa mashine na mitambo. Mpango wa ufufuaji umeanza kwa viwanda vinavyomilikiwa na Chama Kikuu cha Kahama (KACU) na Chama Kikuu cha Chato (CCU).

## Kiwanda cha Chato

Uwezo wa kiwanda ni kuchambua takriban kilo 30,000,000 za Pamba kwa mwaka na kuzalisha marobota 2.5 kwa shift ya saa 8 kila moja. Kiwanda kilisimikiwa cherehani mpya 22 mwaka 2011/2012 aina ya Bajaj inchi 60. Hivyo shift moja huzalisha marobota 55 (22x2.5) na kwa saa 24 marobota 165 (22x2.5x3).



Aidha, mtaji wa ufufuaji wa kiwanda umetokana na mkopo wa wa Tshs. 6,714,804,477.00 (Shilingi bilioni sita milioni mia saba kumi na nne laki nane na nne mia nne sabini na saba tu) toka benki ya TADB.
Hadi tarehe 30 Septemba, 2020 kiwanda kimekwisha chambua pamba kilo 1,165,479 na kuzalisha marobota 2,413 yenye uzito wa wastani wa kilo 181 kila moja. (Kwa wastani wa kiwanda kilo 483 za pamba mbegu huzalisha robota moja). Pamba hiyo iliyo chambuliwa imetoa kilo 697,357 za mbegu. Kwa hali hiyo kila robota moja zalishwa hutoa mbegu kilo 289. Bei ya juu ya mauzo yapamba sufi ni Tshs. 3,000.00 na mbegu Tshs. 531.00.

## Mafanikio Kutokana na Ufufuaji wa Kiwanda

- Wakulima wamelipwa bei zaidi ya bei elekezi toka Tshs. 810.00 hadi Tshs. 900.00 hivyo kupelekea wanunuzi binafsi nao kupandisha hadi kiasi hicho.
- Kuongezeka kwa ajira ambapo kuna shift 3 kiwandani za vibarua 36 kila moja. Jumla yao ni 108 kwa siku. Washushaji na ufumuaji wa mifuko ya pamba watu 20 kwa siku. Hapa kiwandani pameanzishwa migahawa 3 inayotoa huduma ya chakula.
- Watumishi wa kudumu 10 na wa muda 3 hivi sasa wanalipwa mishahara yao kwa wakati.
- Wafanyakazi kuwa na uhakika wa kipato wanawezesha ununuzi wa bidhaa toka kwa wafanyabiashara hivyo kuongeza mzunguko wa fedha na matumizi ya huduma.

## Kiwanda cha KACU

Kiwanda hiki kina jumla ya vyerehani 16, mashine ya kufungia robota na mzani mkubwa wa kidigital wenye uwezo wa kupima kilo 80,000 ambacho kilisimama uzalishaji tangu mwaka 2013/2014. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha robota 48 hadi 50 za pamba nyuzi zenye wastani wa uzito wa kilo 181 kwa kila shift ya masaa nane. Kwa maana nyingine kinazalisha robota 144 hadi 150 kwa siku na hivyo kuwa na uwezo wa kuzalisha robota 3,744 hadi 3,900 kwa mwezi. Uzalishaji huu ni sawa na kuchakata pamba mbegu kilo 1,789,448 mpaka kilo 1,864,008 kwa mwezi.

Chanzo cha mtaji wa kufufua Kiwanda umetokana na mkopo wa jumla ya TZS 4,650,000,000/= (Billioni nne, milioni mia sita hamsini tu) ulioridhiwa na TADB ili kufanya ukarabati wa kiwanda, ununuzi wa pamba mbegu na uchakataji wa pamba mbegu ili kuzalisha pamba nyuzi na mbegu za pamba.

## Mafanikio Kutokana na Ufufuaji wa Kiwanda

- Uchakataji wa pamba mbegu, mpaka tarehe 02/10/2020 kilo 1,230,724 ambazo zimezalisha robota 2,575 za pamba nyuzi zenyewastani wa kilo 181 kwa kila robota na mbegu za pamba kilo 710,347.
- Chama kimepata mnunuzi wa pamba nyuzi kampuni ya Afrisian Ginning Co.Ltd kwa bei ya senti 59 za dola za kimarekani kwa kila ratili ya pamba nyuzi.Hii ni sawa na dola 1.301 kwa kila kilo moja ya pamba nyuzi. Pia tumepata mnunuzi wa mbegu za pamba kampuni ya Kahama Cotton Company Ltd (KCCL) ambayo inanunua mbegu za pamba kwa bei ya TZS 550/= kwa kila kilo.
- Matarajio yetu ni kupata kilo 859,145 za pamba nyuzi ambazo ni sawa na robota 4,747 zenye wastani wa kilo 181, na mbegu za pamba kilo 1,341,010.
- Kiwanda kimetengeneza ajira zipatazo 105 kama vibarua kwa shifti zote tatu, pia ajira za muda maalumu kwa mafundi 12. Wafanyabiashara ndogondogo na mama lishe wanaozunguka kiwanda hiki nao pia wamenufaika.




# MIFUMO YA KUWEZESHA UPATIKANJI WA FEDHA KWA VYAMA VYA USHIRIKA WA NYUMBA

## 1.0 Utangulizi

Katika toleo lililopita ambalo lilikuwa linaangazia uhamasishaji wa ushirika wa nyumba. Katika toleo Makala hiyo, tuliona kuwa nyumba ni mojawapo ya mahitaji muhimu ya binadamu ili aweze kuwa na afya bora na kushiriki vyema katika shughuli za uzalishaji mali. Vilevile tuliona kuwa Vyama vya Ushirika wa nyumba ni njia muhimu ya kuwezesha wananchi wa kipato cha chini waweze kupata makazi bora. Mwisho wa makala nilidokeza mifumo miwili inayoweza kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba kwa vyama vya ushirika wa nyumba. Mifumo hiyo ni Mfadhili – Mjenzi (M-M) na Uanzishaji wa Mifuko ya ujenzi wa nyumba za gaharama nafuu. Hivyo, katika makala hii tutaangalia mfumo mmoja.

## 2.0 Mfumo wa Mfadhili- Mjenzi

Mfumo wa Mfadhili- Mjenzi (M-M) ni mfumo mpya sana katika nchi yetu, lakini unaweza kuwa ni wenye manufaa makubwa katika kuwezesha vyama vya Ushirika wa nyumba kujenga nyumba kwa ajili ya wanachama wake. Hivyo, mfumo huu unajieleza vizuri katika kielelezo kifuatacho hapa chini.




### Kielelezo Na. 1: Mfumo wa Mfadhili - Mjenzi

Kutokana na kielelezo hapo juu, mfumo unahusisha hatua kuu mbili ambazo ni hatua ya ujenzi wa nyumba na hatua ya kufanya malipo ya mkopo wa nyumba. Mfumo unahusisha wahusika wawili wawili katika hatua zote mbili.

## 2.1 Hatua ya kwanza

Hatua ya kwanza inahusisha Chama cha Ushirika wa Nyumba na Mfadhili -Mjenzi. Kila mmoja ana wajibu wake ili mfumo huu uweze kufanya kazi vizuri na kuleta matokeo yaliyokusudiwa. Kwa Chama cha Ushirika wa Nyumba kinatakiwa kuwa kimepata ardhi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wanachama wake na kupata umiliki, ikiwa ni umiliki wa chama ama ni umiliki wa mwanachama mmoja mmoja. Chama kinatakiwa kufanya upembuzi yakinifu (feasibility study) wa mradi wa ujenzi wa nyumba ambapo pamoja na mambo mengine utahusisha tathmini ya uwezo wa mwanachama kulipia gharama ya nyumba (Affordability assessment) bila kuathiri mahitaji mengine muhimu.

Ili kuwezesha upembuzi huo kufanyika vizuri chama kinaweza kuruhusu kazi hii ifanywe na mtoa huduma mwingine ambaye kutoka nje ya chama ili taarifa na takwimu sahihi kwa ajili ya uamuzi juu ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba. Chama Cha Ushirika wa Nyumba pia kitatatakiwa kuwa na ramani za nyumba pamoja na gaharama zote za ujenzi wa nyumba ambazo zimetayarishwa na watu walioidhinishwa kufanya shughuli hizo na zikiwa zimekubaliwa na wanachama kutokana na tathmini ya uwezo wa kulipia gharama za nyumba. Chama pia kitatakiwa kuwa na vibali vya ujenzi kutoka kwenye mamlaka zinazohusika. Aidha, chama kitatakiwa kuwa na hati ya ukomo wa madeni kutoka kwa Mrajis wa vyama vya ushirika kama ambavyo imeelekezwa katika kifungu Na.73 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013.




*Moja ya nyumba zilizojengwa na Ushirika wa Nyumba Mwenge, mkoani Dar Es Salaam*

Baada ya hapo chama kinamtafuta Mfadhili- Mjenzi M-M. Kwa ujumla M-M Kampuni inayohusika na Uendelezaji Miliki na kusajiliwa kwa mujibu wa sheria. M-M anakuwa tayari ana mtaji kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za wanachama wa Chama cha Ushirika wa Nyumba. M-M ana wajibu wa kufanya uhakiki wa mradi wa ujenzi (project appraisal) kwa kuhuisha vitu vyote kuanzia kwenye viwanja ambako nyumba zinatarajiwa kujengwa, kuhakiki michoro yote ya eneo, ramani za nyumba, gharama za ujenzi pamoja na taarifa ya uwezo wa wanachama kumudu gharama za nyumba ( housing affordability assessment report) . M-M atafanya makubaliano na chama cha ushirikia kwa kufuata matakwa ya sheria ya vyama vya ushirika kuhusu uingiaji wa mikataba. Baada ya mkataba kupitishwa, chama kitatakiwa kutoa kiasi cha asilimia 10 au 20 ya fedha zote za ujenzi kutegemea na mkataba kama malipo ya awali. Fedha hizi zinakuwa zimetoka kwa wanachama kutegemea na gharama ya nyumba ya kila mwanachama.

M-M pia atakuwa na wajibu wa kuonyesha wakala wake ambaye atakuwa anakusanya malipo ya mkopo kutoka kwenye chama kwa niaba yake. Chama kinapaswa kufahamu Taasisi ya fedha ambayo itakuwa ni wakala wake na taratibu zote za malipo ya fedha kwa Wakala huyo zitatakiwa kuoneshwa kwenye mkataba. Wajibu mkubwa wa M-M katika hatua ya hii ya kwanza ni kujenga nyumba za wanachama wa chama cha ushirika wa nyumba kwa masharti ya mkataba na kwa viwango vilivyokubalika na baada ya kukamilisha ujenzi huo na chama kuridhika, atakabidhi nyumba hizo kwa chama cha ushirika wa nyumba na hapo ndipo uhusiano wake na chama cha Ushirika wa Nyumba utakuwa umekoma.

## 2.2 Hatua ya pili

Hatua hii inahusu ulipaji wa mkopo wa nyumba na kuwasilisha fedha kwa M-M. Kutokana na makataba, kama mkopo utakuwa ni wa miaka 10 au 15 chama kitakuwa kinalipa fedha kidogo kidogo kila mwezi ambazo zitakuwa zinakusanywa kutoka kwa wanachama na kuwasilisha kwenye taasisi ya fedha ambayo ndiyo itakuwa ni Wakala wa M-M. Wajibu wa Taasisi ya fedha itakuwa ni kukusanya fedha za marejesho ya mkopo na kuwasilisha kwa M-M kwa muda utakaokuwa umeainishwa kwenye mkataba ikiwa ni miezi mitatu au sita kadri itakavyokuwa.
Ndugu Msomaji, tutaendelea kuangalia mfumo mwingine katika makala itakayofuata.

*Mwandishi wa Makala hii ni Afisa Programu Mwandamizi kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU), Ofisi ya Dodoma. Simu: +255 764 021 915*

# MWONGOZO WA MAKISIO YA MAPATO NA MATUMIZI KUSAIDIA USIMAMIZI KATIKA VYAMA VYA USHIRIKA

Dhamira ya Tume ni kusimamia kikamilifu uendeshwaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Misingi ya Ushirika, Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Sekta ya Ushirika. Aidha, usimamizi thabiti hupelekea kuimarika kwa Vyama vya Ushirika sanjari na kutengeneza ushirika endelevu na wenye nguvu kiuchumi unaokidhi mahitaji ya wanachama wake ili kufikia malengo ya uanzishwaji wake.

Mwongozo wa Makisio ya Mapato na Matumizi unatoa ufafanuzi wa kina juu ya uandaaji na uwasilishaji wa maombi ya kuidhinishiwa makadirio ya bajeti ya Vyama vya Ushirika vinavyojishughulisha na biashara ya mazao kama Kanuni ya 62 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 inavyoelekeza, mipango ya bajeti za maendeleo pamoja na Ukomo wa Madeni kama Kifungu cha 73 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika Namba 6 ya mwaka 2013 na Kanuni ya 64 ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015 zinavyoelekeza. Lengo lake ni kutaka kuinua kiwango cha uwajibikaji kwa watendaji na wasimamizi wa shughuli za vyama ili kuongeza tija katika uendeshaji na utekelezaji wake. Aidha, utekelezaji wa matakwa ya mwongozo wa Makisio ya mapato na matumizi, utakwenda sambamba na utekelezaji wa matakwa ya mwongozo wa uhasibu hususan katika Vyama vya Ushirika wa mazao.

Kuwepo kwa mwongozo huu, kutawezesha Vyama vya Ushirika wa mazao kutoa taarifa zenye matokeo ya mwisho juu ya uendeshwaji wa shughuli za kila siku sambamba na kuwezesha wasimamizi wa Vyama vya Ushirika hivyo kufanya udhibiti kulingana na matakwa ya mwongozo huu. Aidha, wadau wote wa ushirika wanatakiwa kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuwa tayari watakuwa wameweza kupata uelewa wa pamoja kupitia mwongozo huu. Mwongozo huu umetayarishwa kwa kuzingatia miongozo mbalimbali iliyowahi kutolewa na wadau, uzoefu, changamoto pamoja na mafanikio ambayo yamekuwa yakipatikana katika Sekta ya Ushirika hususan katika mazao yanayopitia katika mfumo wa Ushirika.

Uandaaji wa makisio ya Vyama vya Ushirika vya mazao, utawezesha watendaji wa vyama hivyo kutunza vitabu vya hesabu, kufunga hesabu na kutoa taarifa muhimu na sahihi kwa wanachama pamoja na wadau kwa ajili ya matumizi mbalimbali. Pamoja na hilo, utaongeza pia ufanisi katika vyama husika sanjari na kumwezesha mwanachama mmoja mmoja kutambua kama chama chake kinaendeshwa kwa faida au hasara, kinadai na kudaiwa, na pia kama kinamiliki mali na madeni hususan wakati wa kujadili na kupitisha makisio hayo katika mkutano mkuu wa mwaka.

Kwa mujibu wa Kanuni Namba 62(1) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika, Chama cha Ushirika kinatakiwa kuandaa na kuwasilisha kwa Mrajis Msaidizi au Mrajis wa Vyama vya Ushirika Makisio ya mapato na matumizi ya kawaida, makisio ya mpango wa bajeti ya maendeleo pamoja na Ukomo wa Madeni kwa msimu husika miezi miwili (2) kabla ya msimu husika kuanza. Baada ya Makisio hayo kupitishwa na wanachama kupitia Mkutano Mkuu kwa mujibu wa Masharti ya Chama, Sheria ya Vyama vya Ushirika pamoja na Kanuni zake, huwasilishwa kwa Mrajis Msaidizi katika eneo/mkoa husika au kwa Mrajis kwa hatua za uidhinishwaji baada ya kukidhi vigezo vilivyowekwa kwa mujibu wa mwongozo huu.

Hatua zifuatazo zinapaswa kuzingatiwa na Vyama vya Ushirika wakati wa uandaaji wa makisio: Uandaaji katika ngazi ya mwanachama; Uandaaji wa makisio katika ngazi ya Chama cha Ushirika cha Msingi (AMCOS); na Uandaaji wa makisio katika ngazi ya Chama Kikuu cha Ushirika au Ushirika wa Mradi wa Pamoja.

Makisio ni makadirio ya kiuchumi ya mapato na matumizi katika Chama cha Ushirika kwa muda maalum kama mwaka/msimu mmoja. Makisio ya Chama cha Ushirika yatazingatia msimu wa zao wa chama hicho.
Kwa mujibu wa Kanuni ya 62(1) ya Kanuni za Vyama vya Ushirika za mwaka 2015, Chama cha Ushirika kinatakiwa kuandaa na kuwasilisha kwa Mrajis Msaidizi au Mrajis wa Vyama vya Ushirika Makisio ya mapato na matumizi ya kawaida pamoja na makisio ya maendeleo kwa msimu husika miezi miwili (2) kabla ya msimu husika kuanza. Baada ya Makisio hayo kupitishwa na wanachama katika Mkutano Mkuu kwa mujibu wa Masharti ya Chama, Sheria pamoja na Kanuni zake, huwasilishwa kwa Mrajis Msaidizi wa mkoa husika au kwa Mrajis kwa hatua za uidhinishwaji.
2.3. Aidha, ili kuweza kumshauri vyema Mrajis au Mrajis Msaidizi kuidhinisha au kutoidhinisha maombi ya makisio ya mapato na matumizi ya kawaida ya Vyama vya Ushirika vya mazao, weledi unatakiwa kutumika ikiwa ni pamoja na kujiridhisha ipasavyo katika maeneo mbalimbali.



*Kikao cha Kujadili na Kupitisha Makisio ya Chama Kikuu cha Ushirika TAMCU*

www.ushirika.go.tz ushirika@ushirika.go.tz ushirika_tcdc
@ushirika_tcdc Tume ya Mendeleo Ushirika

*"Ushirika-Pamoja Tujenge Uchumi Imara na Endelevu"*